# Athari za kubadilisha sera za uhamiaji kwa wateja wa IRC: Maswali ya mara kwa mara

*IRC imejenga rasilimali kwa wateja walio Marekani. Tunatarajia itawasidia watu kuelewa wima haki zao na mchakato wa uhamiaji. Walakini , habari hii sio mbadala ya ushauri wa kisheria kutoka kwa wakili waliohitimu au mwakilishi wa kisheria aliyebainishwa. Habari hii ni sahihi kufikia **Februari 10, 2026** na inaweza kubadilika haraka kwa sababu za mabadiliko zaidi ya sera na/au uamuzi wa mahakama*

## Sera mpya za uhamiaji zitaniathiri vipi?

Sera za uhamiaji zinabadilika haraka na zinaathiri takrbani wote wasio raia wa Marekani. Kila mtu ana hali yake ya kipekee na ni wakili wa uhamiaji tu au mwakilishi wa Idara ya haki-aliyeidhinishwa anayeweza kutoa ushauri kwa hali ya kibinafsi na chaguzi . Hapa chini ni habari ya ujumla inayoweza kukusaidia kukuelekeza kwenye mwekeleo sahihi. Lakini la muhimu sana kushauriana na mwanasheria aliye na leseni ya utendaji kwa ushauri wa hali yako binafsi.

### Mimi ni **mkimbizi.**Je nina hatari ya kupoteza ulinzi wangu au kuondolewa nchi kulingana na misingi ya sera hizi mpya za uhamiaji?

Hali ya ukimbizi ni ya milele. Walakini, mnamo Novemba 21,2025, serikali ya Marekani ilitoa sera mpya inayobidi kukaguliwa upya na uwezekano wa kuhojiwa tena kwa wakimbizi waliopokelewa Marekani kati ya Januari 20,2021 , na Februari 21,2025. Kama uliingia Marekani kama mkimbizi kwa wakati wa kipindi hiki, inapendekezwa uwasiliane na wakili wa uhamiaji kuhusu kesi yako na jinsi ya kujiandaa kwa uwezekano wa mahojiano. Unaweza kupata habari zaidi hapa”here. “

### Je **natoka nchi moja kati ya zilizo katika orodha ya “kupigwa marufuku” kusafiri.** Je, nina hatari ya kupoteza ulinzi au kuondolewa kutegemea sera hizi mpya za uhamiaji?

Mnamo Desemba 2, 2025, seriakali ya Marekani ilitoa sera mpya inayotoa uwezekano wa kuhojiwa tena kwa watu wote walioingia Marekani kati au baada ya Januari 20.2021 kutoka mojawapo ya nchi 19 zilizopigwa “marufuku ya kusafiri” .Sera hii ilipanuliwa Januari 2,2026 kujumilisha nyogeza ya nchi 20. Kama wewe ni raia wa nchi mojawapo ya nchi hizi na uliingia Marekani kati au baada ya Januari 20,2021, unaweza fikiria kushauriana na wakili wa uhamiaji kuhusu kesi yako.. Pata habari zaidi hapa”here”.

### Niko na hali ya ulinzi wa muda **“Temporary Protected Status”** (TPS) au Msamaha wa kibinadamu. **“Humanitarian Parole”** Je, nina hatari ya kupoteza ulinzi au kuondolewa kwa msingi wa sera hizi mpya?

Serikali ya Marekani ilitamatisha TPS kwa nchi nyingi zilzizokuwa mbeleni zimeteuliwa. Kama TPS imekatishwa, wale kwa sasa wana TPS hawataweza kupata upy TPS au kadi ya kutumika kazi na wanaweza kulengwa kwa kutiwa kizuizinin au/na kuondolewa. Tafadhari angalia hapa “” here” kuhakiki orodah ya sasa ya nchi zilziobakia kama teule kwa TPS na tarehe sahihi za uhalali wa kila mojawapo.

Msamaha umekatizwa kwa watu wengi walioingia Marekani kwa hali ya msamaha wa kibinadamu. Kama kwa sasa una hali ya msamaha unapaswa haraka sana kutafuta usaidizi wa kisheria kukagua ikiwa unaweza kuomba usamehevu tena au kupeleleza chaguzi mbadala za kisheria na ulinzi wa kutoondolewa.

## Ni hati gani napaswa kubeba nami?

**Tahadhari:** Ina pendekezwa kubeba kila wakati hati asilia au nakala zake nawe. Hakikisha una nakala za ziada katika mahali salama nyumbani

| Hali | Hati unazopaswa kubeba nawe |
|---|---|
| kama una **hali ya sasa ya uhamiaji** | **Kila wakati beba hati zitakazoonyesha dhibitisho una hali ya ukmibizi Marekani , kama vile:**<br>1. **I-551** dhibitisho la uhalali wa ukaaji wa kudumu (Green Card)<br>2. **I-94** dhibitisho la uhalali wa kuingia au pasipoti iliyopigwa mhuri au hati za usafiri yenye visa au/mhuri wa kuingia.<br>3. **Kadi ya kibali cha ajira"Employment Authorization Card"** (kibali cha kazi)<br>4. **I-797** notisi ya kuidhinishwa hali yako ya uhamiaji<br>5. **Leseni ya udereva ya Jimbo**—kama tu Jimbo lako linahitaji hali yako ya wakati uliopo kupata leseni ya udereva. |
| Kama **hali yako inasubiria**(kumaanisha umetuma ombi kwa manufaa ya uhamiaji au ulinzi lakini huna matokeo ya kesi yako) | Beba **nakala za resiti kutoka USCIS (I-797)**.<br><br>**Tahadhari**: kuwa na ombi la hali linalosubiria halikupi ulinzi kutokana na kuwekwa kizuizini au kuondolewa |
| Kama uko katika **mchakato wa kuondolewa na huna kadi ya kutumika kazi** | Beba nakala ya resiti yako **Notisi ya kusikizwa** ,**resiti** yoyote unayoweza kuwa nayo ya kutuma ombi au, **notisi ya msamaha**(inapohusika). |
| kama **hujasajiliwa** | **USIBEBE nakala** za vitambulisho au pasipoti ya kitaifa kwani zinaweza kutumiwa kinyume nawe na mahakama ya uhamiaji.<br>**Tahadhari**: Usibeba hati zozote za uongo au hati za mtu mwingine |
| Kama **hujasajiliwa** au **hali yako inasubiria**, wewe **haupo kwenye mchakato wa kuondolewa,NA umekuwa Marekani kwa zaidi ya miaka 2** | Beba **thibitisho la uwepo wa kiwili** Marekani kwa miaka 2 na kuendelea kujilinda dhidi ya kuondolewa kwa haraka.<br>**Tahadhari**: Haya hayakulindi kikamilifu kuzuiliwa au kuondolewa lakni yanaweza kukulinda kutokana na kuondolewa kwa haraka<br>Hii ni Pamoja na nakala za hati zifuatazo:<br>• Dhibitisho la kukamilisha ushuru kwa miaka mitatu(ni ITIN halali au namba ya Social Security iliyotumika)<br>• Hati za kodi ya nyumba<br>• Ada za matumizi ya umeme<br>• Rekodi za shule yako au ya watoto<br>• Hati zozote unazoweza kuwa nazo zinazoweza kudhibitisha uwepo wako Marekani kwa zaidi ya miaka 2. |

# ELEWA HAKI ZAKO!

Watu wote wanaoishi Marekani, bila kujali hali zao za uhamiaji, wana haki chini ya Katiba ya Marekani.

Kama umesimamishwa au  umulizwa maswali na polisi au ofisa wa uhamiaji, kumbuka kuwa **una haki zifuatazo:**

- **Unaweza kukataa kuzungumza**. Si lazima useme mahali ulikozaliwa au jinsi ulivyoingia Marekani.
- Kama wewe si raia wa Marekani na ofisa wa uhamiaji aombe hati,lazima umwonyeshe kama unazo nawe. Kila wakati beba hati zako za uhamiaji**.Kama huna hati za uhamiaji, sema unataka kukaa kimya**
- Kama uko nyumbani **si lazima uwaruhusu wakala wa utekelezaji wa sheria ila tu wanapokuonyesha hati ya mahakama, iliyotiwa sahihi najaji au hakimu.**
- **Una haki kuzungumza na wakili**.
- **Kabla ya kutia sahihi yoyote,zungumza na wakili**
- **Beba kadi nyekundu ya elewa haki zako”** Know Your Rights Red Card **“ kwa lugha yako** Na uonyeshe ofisa wa uhamiaji akikusimamisha.

## Tafadhari tumia utandu uliopo hapa chini **kupata habari zaidi** jinsi ya kulinda haki zako:

**Kadi nyekundu ya ILRC”** ILRC Red Cards”

**Tunahaki.us”Wehaverights.us”**

## Kujiandaa kwa hali za **dharura**, ikiwemo kutiwa kizuizini au kutenganishwa na wapendwa wako:

Kuwa tiyarisasa!" **ReadyNow!**" ni jukwaa la bure na salama na hutumika kwa jukwaa za simu limiundwa kusaidia wahamiaji kujiandaa kwa uwezekano wa kutiwa kizuizini na kutenda kwa haraka katika hali za miharuko kwa kuwatahadharisha rafiki na familia kwa habari muhimu wanazotakiwa kujua kama umezuiliwa na watekelazaji wa sheria. Jukwaa hili lina lugha mbalimbali.

1. **Mfumo wa dharura wa mpigo mmoja** Kifaa cha tahadhari hutaharisha mara moja walengwa wako wa dharura na waakilishi wako wa kisheria kuhusu mipango yako ya dharura iwapo umezuiliwa na mamlaka ya uhamiaji
2. **Upangaji wa dharura uliorahisishwa**. Mipango yako ya dharura ni mfululizo wa jumbe zinazotumwa kwa utandu wako wa msaada ikiwa pana kuzuiliwa na mamlaka ya uhamiaji

    - Kwanza unda ujumbe halali saidizi. Huu utatumwa kwa wakili wa uhamiaji kama uko naye. Kama huna, unaweza kuchagua kushirikisha Habari zako na mtandao wa mawakili.
    - La pili, unda ujumbe wa ulinzi wa binafsi kwa rafiki au famiia ya karibu. Hii itabeba habari wanapaswa kuelewa kukupata na kutete kwa naiba yako. Tiyarisasa! "ReadyNow!" inapendekeza ujumlishe jina na jinsi ya mawasiliano na wakili wako(kama unaye), namba yako ya uhamiaji(A-number) na utandu wa kuwatafuta wazuiliwa wa ICE ili wapendwa wao waweze kuwasilana nao, Habari muhimu kuhusu afya yako, na mahali hati zako muhimu zimehifadhiwa.

    - La tatu, unda jumbe zaidi tofauti kuhusu ulezi wa Watoto, wakongwe, Wanyama , na kukisia kutofika kazini. Kila ujumbe,kama ulichagua kuunda,utatumwa kwa walengwa. Elewa kuwa unaweza kutamani kushirikisha mipango yako ya dharura kwa familia na marafiki kabla ya kubonyesha kidunde cha tahadhari. Jukwaa la Tiyarisasa!" ReadyNow!"hutoa chaguo la kushirikisha nakal a za mipango ya dharura na walengwa muhimu mapema.

3. **Kuunganishwa na usaidizi wa kisheria**. Unapoandaa mpango wako wa dharura,utakuwa na nafasi ya kutoa kibali kushirikisha habari zako na mtandao wa watoa huduma za kisheria za uhamiaji na watetezi wanaokabiliana na dharura. Ikiwa utachagua chaguo hili na uamilishe tahadhari, habari zako zitashirikiswa na mtandao wa kitaifa wa usaidizi wa kisheria,utakao jaribu kukuunganisha na waakilishi aminika wa kisheria . tafadhari elewa kuchagua chaguo hili hakukupi dhamana kuwa utawekwa chini ya wakili wakati wa kuzuiliwa,kwani inategemea uwepo wake ,katika eneo, na hasa hasa mahitaji maalumu ya kisheria.

**Ulinzi wa faragha na usalama** . Pokezi zote zimesimbwa, kuhifadhiwa kwenye kifaa cha watuamiaji ,na huvutwa baada ya tahadhari kutumwa, kuzuia kupatikana na maofisa wa serikali kama watachukua simu.

Tiyarisasa! "ReadyNow!" ni pakuo mtandao la bure linalopatikana kwa **Apple App Store** na **Google Play**.

Habari zaidi na rasilimali utakazo penda kushirikisha na familia na marafiki kutayarisha uwezekano wa kutiwa kizuizini na kuwasaidia kushughulika kikamilifu inaweza kupatikana katika mambo m5 unayoweza kufanya kama mpendwa wako amewekwa kizuizini na ICE au walinda doria mipakani“5 Things You Can Do if Loved One is Detained by ICE or Border Patrol”.

## Nawezaje kupata usaidizi wa kisheria na misaada mingine?

Ongea na wakili wa uhamiaji au mwakilishi wa Idara ya haki-aliyeidhinishwa kuhusu chaguzi kama mhamiaji Marekani. Wasiliana na wakili binafsi wa uhamiaji au mtoa huduma za uhamiaji asiyelipwa ili kuelewa chaguzi zako

Unaweza kupekua wakili wa uhamiaji asiyelipwa katika eneo lako kupitia “American Immigration Lawyers Association” au “Asylum Seeker Advocacy Project (ASAP list of private attorneys. Orodha ya huduma ya kisheria ya kitaifa “the National Immigration Legal Service Directory “ pia iko na orodha ya watoa huduma za uhamiaji wasiolipwa wa maeneo. Kwa sababu za uhitaji wa juu, kupata usaidizi haraka kutoka kwa mtoa huduma za kisheria papop hapo panaweza zua changamoto.

Unaweza pitia eneo fikia watoa huduma za dharura wa eneo lako “Rapid Response Network of Hotlines” kwa usaidizi wa dharura,kwani mitandao hii haswa **hujumlisha huduma pana za misaada ya jamii**.

**Kuepuka kashfa za uhamiaji!**

**Uliza uzoevu wa kisheria za uhamiaji alio nao wakili au mwakilishi wa DOJ aliyeidhinishwa anayekusaidia**

- Kumbuka kuwa ni mawakili wa uhamiaji pekke na waakilishi walioidhinishwa wanaoweza kutoa ushauri wa kisheria. Tahadhari walaghai sugu au watoa huduma za umma wasioidhinishwa au kufaulu kutoa ushauri wa uhamiaji. Watakupotezea wakati na pes ana wanaweza kutia kesi katika adhari mbaya.
- Kabla ya kuajiri yeyote akusaidia na kesi yako, uliza hati za ustahiki wao. Je ni wakili au mwakilishi aliyeidhinishwa? Ana uzoevu upi wa sheria za uhamiaji? Bonyeza utandu huu kwa habari zaidi kuhusu kashfa za uhamiaji Immigration Scams.

Tafadhari tumia utandu uliopo hapa chini kupata **usaidizi wa kisheria** katika mji wako:

| Mtandao wa watetezi wa uhamiaji"Immigration Advocates Network | Chama cha wanasheria wa uhamiaji wa Marekani"American Immigration Lawyers Association | Orodha ya ASAP ya wanasheria binafsi ASAP list of private attorneys | Mtandao wa dharura wa majibu ya haraka<br><br>wa simu za dharura Rapid Response Network of Hotlines | **Muhimu mimi "ImportaMí'** *(kwa **vijana** walioingia Marekani bila kuandamana na wazazi au mlezi wa kisheria)* |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |